# Inafananaje **Kuomba** kwa Bidii?



PASTOR JAMES KALEKWA

# INAFANANAJE KUOMBA KWA BIDII?

James Kalekwa

## Yaliyomo katika Bidii:

Salamu za Mama Mchungaji JK. ....... 4

Mwitikio wa asili wa mwamini ni kuomba!................................................ 6

Mguso wa kibinafsi wa ndani...........12

Maazimio kutokea ndani ...................18

Matumizi ya maneno yanayomaanisha ...................................24

Kushughulisha/Kuhusisha utendajikazi mwili..............................34

Muda mrefu – Kushikilia ajenda moja ya maombi kwa muda mrefu!...........38

Kilio na Machozi .................................44

Kuhusu Mwandishi:...........................50

Kuhusu New Vine Church: ...............51

Mawasiliano na Mwandishi:............52

## Salamu za Mama Mchungaji JK.

Juni 20, Mungu alitupa zawadi ya maisha ya mtumishi wake Pastor JK, mtu wa juhudi nyingi katika Kristo na maarifa ya kimungu. Kwa muda ambao nimekuwa naye kwenye maisha, nimemtambua kama mtu anayempenda Mungu kiasi cha mimi kukosa neno la kuelezea. Huyu ni mtu aliuzwa kwa Mungu na utumishi!

Amewekeza muda mwingi kuandika mfululizo wa vitabu hivi vya kielektroniki ili avitoe bila malipo kama sehemu yake ya ujenzi wa mwili wa Kristo… kwa niaba yake, ninaomba ukipokee kwa kuthamini dhabihu! Ninakuombea ya kwamba maisha yako yanageuzwa kwa kitabu hiki kimoja tu kwa jina la Yesu Kristo.

Pili, ninaomba uwasambazie kitabu hiki watu wengi zaidi ili maono ya kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari yatimilizwe.

Na hatimaye, kwa kuthamini zawadi ya mtu huyu wa Mungu, muombee, mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumsherehekea ukimweleza namna gani umesadika na utumishi wake – itafaa sana.

Heri ya siku ya kuzaliwa mume wangu mpenzi. Heri ya kuzaliwa Pastor JK – zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu!

Frida James Kalekwa (Mama mchungaji JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2025
Dodoma, Tanzania

## Mwitikio wa asili wa mwamini ni kuomba!

*"Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa.* ***Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.****"* Yakobo 5:16

Ni vizuri sana kuambiwa uombe! Na vizuri zaidi ukielekezwa uombe namna gani. Uonyeshwe mfano; uonyeshwe inafananaje kuliweka hilo agizo kwenye hatua za utekelezaji.

Mtume Yakobo, sehemu kubwa ya maandiko yake, amevuviwa na Roho Mtakatifu kuonyesha namna ya kuuishi ukristo; namna gani ya kuutekeleza

ukristo. Sehemu hii ya andiko anatufunulia namna ya kuomba – kwa vitendo!

Kwenye sura hii ya 5 kuanzia mstari wa 13 mpaka 18 anatambulisha dhana ya maombi na kuonyesha namna gani inafaa kutekelezwa. Anasema mtu aliyepatikana na mabaya (dhiki/majaribu) – ayaitikieje mabaya hayo; mtu ambaye haweza (mgonjwa) – auitikieje ugonjwa huo; na watu wote wanaoenda kuwahudumia wanaopita kwenye magumu hayo (majaribu au magonjwa) wanapaswa kuitikiaje… ni kwa kuomba!

Aliyepatikana na mabaya – Aombe!

Aliye hawezi – Aombe!

Wazee wa kanisa wanaowahudumia – Waombe!

Mwitikio wa asili wa mwamini kwenye hali zote ni kuomba!

Kisha anasogea mbele kuonyesha namna gani ya kuomba kwa kuongeza neno **bidii** ambalo halikuwepo hapo awali! Kisha mstari wa 17 na 18 anatupa taswira ya bidii kwa kurejelea namna ya maombi ya Eliya na matokeo yake.

Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi… yaani, alikuwa anapatikana na mabaya na alikuwa kuna nyakati hawezi! Lakini angalia matokeo aliyoamuru katika madhabahu ya maombi si kwa sababu ya kuomba tu bali ni kwa sababu ya bidii aliyohusisha kwenye maombi.

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 4) ya TATAKI, bidii ni *ari ya kufanya jambo*. Visawe vya neno bidii ni: **jitihada, hima, kasi, juhudi, hamasa** (kwa faida ya wasiofahamu: kisawe ni neno lenye maana ileile ya

neno linguine kwa kimombo ni synonym).

Kuomba kwake mwenyehaki kwa faa sana akiomba kwa ***bidii, jitihada, hima, kasi, juhudi, hamasa!*** Je, kwako haya yanasikika kama maneno mepesi narahisi tu? Je, ni maneno ya kawaida?

Binafsi ningetamani sana kuona na kuiga kuomba kwa bidii kunafananaje.

Kwa kuwa tumepewa mfano wa Eliya aliyekuwa na tabia kama yetu, inabidi twende kutafiti bidii yake ya kuomba. Kwenye kitabu cha 1 Wafalme 17 na 18 zote. Lakini mkazo hasa uko kwenye

18:42-45. Kutokea humo tunachota mwonekano kadhaa wa kuomba kwa bidii ambao nitautumia na kuongezea rejea zingine au mifano mingine kutoka sehemu zingine za Maandiko ili kuujenga uelewa wako kwa nguvu ya neno la Mungu.

Unapoendelea kujifunza, nimekuombea ya kwamba namna yako ya kuomba itabadilishwa mara tu baada ya kusoma kitabu hiki. Ninaona shujaa wa maombi ambaye ni wewe anainuka na kuomba kwa bidii katika jina la Yesu Kristo.

## Mguso wa kibinafsi wa ndani.

Kwa neno hili ninawasilisha dhana ya hali ya kushawishika kibinafsi kutokea ndani yako. Na hapo ndipo bidii ya maombi huzaliwa.

Unaweza kualikwa kwenye mkutano wa maombi; Unaweza kukaribishwa kwenye mkesha wa maombi; unaweza kuungana na waamini wanaoomba. Lakini kama wewe haujashawishika kibinafsi kutokea ndani yako kuhusiana na uhitaji wako wa kuomba nay a kwamba hiyo ndiyo namna pekee ya kushughulika na jambo hilo, bidii haiwezi kuzaliwa!

Mathayo 26:38, *"Ndipo akawaambia, **Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa**; kaeni hapa, mkeshe pamoja nami."*

Unaona maombi yalikoanzia? Ni kwenye roho yake… imekuwa na huzuni nyingi kiasi cha kufa! Siyo amealikwa tu. Siyo ameona mlima wa maombi. Kuna kitu kinaendelea kutokea ndani mwake. Sasa, tazama kwenye Maandiko ni kwa jinsi gani hiyo hali ya ndani ilisukuma bidii ya nje ya kimaombi.

Luka 22:44 (SUV), "*Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki, akazidi sana*

*kuomba; hari yake* ***ikawa kama matone ya damu*** *yakidondoka nchini.]"*

*"Akiwa katika uchungu mkubwa,* ***alisali kwa bidii zaidi; na jasho likamtoka kama matone ya damu****, likatiririka mpaka chini."* – BHN

*"…****maumivu makali****…"* (NEN)

Bidii ilipelekea siyo tu maneno yatoke… siyo jasho litoke… DAMU ilimwagika! Je, unaweza kuwa na mashaka kwamba kuna machozi yalimwagika? Sasa, nifuate vizuri hapa. Sisemi ya kwamba lengo lake lilikuwa ni kumwaga damu katika maombi. Bali msukumo wa nguvu

wa kimaombi ndiyo ulipelekea damu kutoka!

Ukiwa umeshikwa na jambo ndani ya moyo wako, mwili huitikia sawia.

Hebu tutazame mfano wa mtu mwingine na kipengele hiki cha kushawishiwa kwa namna ya ndani.

1 Sam 1:7-8,10, *"Tena mumewe akafanya hivyo mwaka kwa mwaka, hapo yule mwanamke alipokwea kwenda nyumbani kwa BWANA, ndivyo yule alivyomchokoza; basi, kwa hiyo, yeye akalia, asile chakula. 8Elkana mumewe akamwambia, Hana, unalilia nini?*

*Kwani huli chakula? Kwa nini moyo wako una huzuni? Je! Mimi si bora kwako kuliko watoto kumi?* ***10. Naye huyo mwanamke alikuwa na uchungu rohoni mwake, akamwomba BWANA akalia sana.****”*

Umeona neno “uchungu rohoni mwake…”? Huu mzigo wa kimaombi wa mwanamke Hana haukuwa ni swala la kiufahamu tu… haikuwa *head knowledge*… halikuwa ni taarifa. Lilizaliwa kutokea rohoni mwake. Moyo wake ulikuwa umeshawishika kiasi hicho.

Ndiyo maana chakula hakikufaa wala faraja isingetosha isipokuwa kujimimina tu mbele za Bwana.

Si ajabau kuna namna ya kuomba ambayao Hana anaidhihirisha ambayo mpaka Kuhani Mkuu, Eli anaistaajabia… kimsingi, muhula wake wote wa ukuhani hajawahi kukutana na mtindo huu wa kuomba!

Ukiombea kutoka kichwani utachoka!

Ukiomba kutoka kichwani hutakuwa na bidii!

Inafaa kuanzisha ndani ya moyo kwa kushawishika kibinafsi na si kwa hamasa kutoka kwa yeyote.

Nionyeshe mtu ambaye moyo wake umeshawishika kuhusiana na jambo fulani, nitakuonyesha mtu anayeomba kwa bidii.

## Maazimio kutokea ndani

Hii ni jumla ya maazimio, makusudio, maapizo inayomsukuma mtu kwenda kwenye maombi. Ninaomba mpaka iweje!? Ninaomba mpaka nione nini? Ninaomba ili iweje?

Ni usongo, hamu au hamasa aliyo nayo mtu husika kiasi cha kulazimika kwenda kuomba tu.

Umewahi kusikia watu wanasema, *“Acha tuteme nyongo”? “Acha nitoe ya moyoni”?* – Hiki ndicho kinamaanishwa hapa. Yaani, bila matokeo haya; bila majibu haya; pasipo badiliko hili… sitakuwa nimemaliza kuomba.

Kimsingi namna hii ya bidii huwa haijali sana muda au ratiba bali matokeo/majibu ya maombi. Namna hii ya maombi ni ile huwa ninaiita kuomba kwa utungu kama wa mama mjamzito anayetaka kujifungua… ni kusukuma mpaka mtoto

azaliwe. Ni maombi ya ku-PUSH… Pray Until Something Happens (PUSH)

Hebu tazama mifano kadhaa ambayo nimekukusanyia hapa uone watu wa Mungu alivyojiapiza na kuweka maazimio ya kwamba bila matokeo fulani hawawezi kujihesabu ya kwamba wameomba.

Hapa New Vine Church –Dodoma, ni lugha inayofahamika karibia na kila mshirika ya kwamba ni kiburi cha hali ya juu sana au ni onyesho la ujeuri kulala, kupata usingizi, kula chakula na kushiba wakati kuna agenda za kimaombi

ambazo ulipaswa kuwa umezikamilisha lakini hazijakamilika!

*"Akasema, Niache, niende, maana kunapambazuka.* ***Akasema, Sikuachi, usiponibariki.****"* **Mwanzo 32:26**

*"****Sitaingia hemani mwa nyumba yangu, Wala sitapanda matandiko ya kitanda changu; Sitaacha macho yangu kuwa na usingizi, Wala kope zangu kusinzia****; Hata nitakapompatia BWANA mahali, Na Shujaa wa Yakobo maskani."* **Zaburi 132:3-5**

*"Uende ukawakusanye Wayahudi wote waliopo hapa Shushani, mkafunge kwa*

*ajili yangu; msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana, nami na wajakazi wangu tutafunga vile vile;* ***kisha nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria; nami nikiangamia, na niangamie.****"* **Esta 4:16**

Binafsi nimefika mahali pa utambuzi ya kwamba mara nyingi wanaosema, *"Nami nikiangamia, na niangamie"* huwa hawaangamii wa sababu huwa wamekishinda kinachoangamiza kwenye madhabahu ya maombi!

Umemuona Yakobo? Umemuona Mzaburi, Daudi? Umemuona Esta?

Umeona namna ambavyo dunia yao ilibidi isimame kwanza mpka waone matokeo ya kuomba kwao. Hawakubali kupambazuke bila kubarikiwa; hawawezi kulala na kupata usingizi mpaka wamempatia Bwana nafasi; hawawezi kuishi kwa ufahari tena wakati kuna uangamivu unaendelea.

Mpendwa wangu, bidii itaratibu ratiba zako! Pungufu ya hapo ni maombi ya kidini na kimapokeo tu.

Ninasikia moyo wako umewaka hasira mpaka hapa.

## Matumizi ya maneno yanayomaanisha

Ninataka kutambulisha kwako kanuni muhimu sana hapa. Aawali ya yote ni vyema ufahamu ya kwamba kuomba ni KUSEMA… ni kufungua kinywa na kutamka!

*"Akawaambia, Msalipo,* ***semeni****, Baba [yetu uliye mbinguni], Jina lako litakaswe, Ufalme wako uje, [Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.]"* Luka 11:2

Matamshi yako huonyesha kinachoendelea moyoni mwako… hufunua imani yako. Kuna mambo

ukiona huwezi kuyathubutu kuyaomba, basi huyaamini kuanzia awali.

Mwenye hekima mmoja alisema, *“Washindi ni watu wenye midomo mikubwa.”* Akimaanisha washindi hufungua sana midomo yao katika maombi. Ama kwa hakika kinywa kilichofumbwa, ni hatima iliyofumbwa.

Ninataka kukuonyesha ya kwamba kufumbua kinywa katika kuomba ndiyo hatua ya awali. Hata hivyo, unapofumbua kinywa katika kuomba ni mambo gani hasa unayoyatamka?

Bidii ya maombi huambatana na matamshi ya maneno “hatari sana” ambayo ndiyo yaliyomaanishwa kutokea moyoni na yule aombaye… Hebu tazama vielelzo kadhaa vya kimaandiko amabavyo nimekuorodheshea hapa.

*“Basi Eliya Mtishbi, wa wageni wa Gileadi, akamwambia Ahabu, Kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele zake,* ***hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii, ila kwa neno langu.”*** **1 Wafalme 17:1**

Fikiria mtu anakuja na kusema mvua inategemea rehema zangu! Yeye ndiye aliyeshikilia funguo za mvua… Fikiri!

Huenda unakosa kile ninakimaanisha… Iko hivi, kuna mambo ambayo ni haki za asili za mwanadamu. Kama vile hewa, maji, uhai - hivi havipaswi kuuzwa/kununuliwa. Si unafahamu hata kwenye sekta ya afya huwa hawauzi hewa ya oksijeni bali wanauza mtungi (chombo chochote kwa jiana lake) uliobeba hewa hiyo? Kwa sababu ni haki ya asilia.

Sasa, anakuja mwanadamu anasema yeye ndiye ameshikilia haki ya asili ya

taifa zima! Ni jambo gumu sana. Lakini ndicho kilichomaanishwa.

Zab 22:1 (SUV), *"Mungu wangu, Mungu wangu,* ***Mbona umeniacha? Mbona U mbali na wokovu wangu, Na maneno ya kuugua kwangu?****"*

Zab 143:7 (SUV), *"Ee BWANA, unijibu hima,* ***roho yangu imelegea; Usinifiche uso wako****, Nisifanane nao washukao shimoni"*

*"Ee BWANA,* ***utete nao wanaoteta nami****,* ***Upigane nao wanaopigana nami****."* Zaburi 35:1

*“Ee BWANA, nilie hata lini,* ***wewe usitake kusikia? Nakulilia kwa sababu ya udhalimu, ila hutaki kuokoa****.* ***3Mbona wanionyesha uovu****, na kunitazamisha ukaidi? Maana uharibifu na udhalimu u mbele yangu; kuna ugomvi, na mashindano yatokea. Matumizi ya kunena kwa lugha”* Habakuki 1:2-3

Yer 20:7 (SUV), *“****Ee BWANA, umenihadaa, nami nimehadaika; wewe una nguvu kuliko mimi, ukashinda****; nimekuwa kitu cha kuchekesha, mchana kutwa; kila mtu hunidhihaki.”*

Bidii ya maombi huambatana na maneno ya dhati ya moyo wa mwombaji. Hapa, mtu hatumii misamiati au kuonyesha umaridadi wake wa lugha mbele za Mungu. Huyasema mambo kama yalivyo ndani ya moyo wake.

Kuna maneno ukisoma kwenye Biblia mpaka unajiuliza hivi huyu anajua kwamba hapa alikuwa anamuomba Mungu? Kuna maneno unasoma mpaka unadhani ni mtu anafanya utani na babu yake.

Mistari mingi ya rejea nimekuwekea hapo juu inaonyesha watu wa kweli

mbele za Bwana; mioyo wazi mbele za Bwana.

Kama wamechoka, basi wanasema kwamba “Mungu nimechoka!”

Basi wanasikia hasira, wanasema kwa uwazi, “Mungu nimekasirika!”

Hawaji na misamiati mingi ya kidini na kitheolojia kumuonyesha Mungu ni kwa jinsi gani wanamjua… wanatumia lugha mbichi kama ilivyo. Hakuna nakshi.

Hebu fikiria unamwambia Mungu, *“Ee Bwana umenihadaa*…”. Waza huyu mwingine anaomba anamwambia, *“...roho yangu imelegea, usinifiche uso*

*wako…”;* Mwingine anauliza, *“... nilie mpaka linin a wewe hutaki kusikia… hutaki kuokoa!”*

Sasa, kutokea hapo ninaweza kumwelewa mtu ambaye nafsi yake imechoka na hana tena lugha na misamiati ya kikanisa bali anasema, *“Yesu nibebe… nibembeleze, nibebe!”*. Maadamu ni kilio cha dhati cha moyo wake, Bwana Yesu anamwelewa sana na huja hima na kumtendea sawa na shauku ya moyo wake.

Wataalamu wa maswala ya mahusiano husema ya kwamba, kwa kadiri watu wanavyohusiana kwa ukaribu na kuwa

na muda mwingi pamoja ndivyo ambavyo huwa wanaelewa sana katika lugha kiasi kwamba wanaelewa hata ukimya, sauti, kelele na milio.

Hii hupelekea watu ho kuanza kuongea kwa dhati ya moyo wakijua fika ya kwamba upande unaopokea maneno hayo hautawahukumu bali utawapokea na kuwaelewa vyema sana.

Mtu anaychagua na kupembua sana maneno kwa umakinifu, huenda amekuja kufanya onyesho la maombi mbele za hadhira yake yaani Mungu!

## Kushughulisha/Kuhusisha utendajikazi mwili

Bwana Yesu alielekeza kwamba tunapaswa kumpenda Bwana, Mungu wetu kwa:

- Moyo wako wote
- Roho yako yote
- Akili zako zote
- Nguvu zako zote

Kwa hiyo, Mungu hupendwa kwenye madaraja yote hayo manne. Hivyo katika madhabahu ya maombi, bidii inaonekana katika madaraja hayo pia.

Na hapa, ningependa kuwasilisha mkazo katika daraja la nguvu za mwili au uhusiaka wa moja kwa moja wa mwili. Kwa kuwa, wengi tumeona ya kwamba maombi ni shughuli ya kiroho tu – tumeacha kuhusisha akili zetu, mioyo yetu (hisia na vionjo vya ndani), na miili yetu..

Hebu rejelea maandiko yaliyoambatanishwa hapa kukujengea ufahamu:

> *"Basi Ahabu akainuka ili ale na kunywa. Naye Eliya akapanda juu mpaka kilele cha Karmeli;* ***akasujudu kifudifudi, akainama uso mpaka magotini.****"* **1 Falm 18:42**

Mathayo 26:39, *"Akaendelea mbele kidogo,* ***akaanguka kifulifuli****, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe."*

Haiyumkiniki hata kidogo kwamba una bidii katika kuomba na umesimama wima na kwa mwonekano maombi yako na mwili wako havina ushirikiano.

Kuna matendo ya nje mwilini ambayo huonyesha kinachoendelea moyoni mwako na kiwango chako cha kumaanisha katika uyatendayo. Simaanishi kwenda kwenye ng'ambo

iliyopitiliza (extreme) ya udini na sheria. Hata hivyo, simaanisha vilevile ng'ambo ya pili iliyopitiliza ya umauhuru.

Wataalamu wamamawasiliano hukubaliana kwa pamoja ya kwamba lugha ya mwili ina sehemu kubwa ya uwasilishaji wa ujumbe kuliko hata maneno yanayotumiwa.

Bidii katika kuomba itakuplekea – k*upiga magoti*, *kupomoka kifudifudi*, *kunyoosha mikono*, *kupiga makofi*, *kurusharusha mikono*, *kutembea*, *kupaza sauti*, *kulia*, *kumwaga machozi*, *kuruka*. Huwezi kuiita ni bidii ya maombi wakati

mwili hauhusiki kwa namna yoyote kwenye kinachoendelea.

## Muda mrefu – Kushikilia ajenda moja ya maombi kwa muda mrefu!

Bidii katika maombi huonyesha na muda unaotwekezwa katika kuomba na kushikilia ajenda husika ya kimaombi. Kuna mifano kadhaa ya kibiblia inayoonyesha kiwango cha muda ambao watu mbalimbali waliwekeza kwenye maombi. Utagundua ya

kwamba bidii ya maombi pia huonekana katika uwekezaji wa muda.

Hebu tazama mifano niliyokuambatanishia hapa.

> Mathayo 26:40 *"Akawajia wale wanafunzi, akawakuta wamelala, akamwambia Petro,* ***Je! Hamkuweza kukesha pamoja nami hata saa moja?****"*

> Luka 6:12 *"Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba,* ***akakesha usiku kucha*** *katika kumwomba Mungu."*

> *Yona 1:17, "BWANA akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona* ***akawa ndani ya tumbo la samaki***

***yule muda wa siku tatu, mchana na usiku**.”*

**Yona 2:1,** *“**Ndipo Yona akamwomba BWANA,** Mungu wake, katika tumbo la yule samaki,”*

**Esta 4:16,** *“Uende ukawakusanye Wayahudi wote waliopo hapa Shushani, **mkafunge kwa ajili yangu; msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana, nami na wajakazi wangu tutafunga vile vile**; kisha nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria; nami nikiangamia, na niangamie.”*

**Danieli 6:10,** *"Hata Danieli, alipojua ya kuwa yale maandiko yamekwisha kutiwa sahihi, akaingia nyumbani mwake, (na madirisha katika chumba chake yalikuwa yamefunguliwa kukabili Yerusalemu;)* ***akapiga magoti mara tatu kila siku, akasali, akashukuru mbele za Mungu wake, kama alivyokuwa akifanya tokea hapo****."*

**Danieli 10:2-3***, "Katika siku zile mimi, Danieli,* ***nalikuwa nikiomboleza muda wa majuma matatu kamili****. 3Sikula chakula kitamu, wala nyama wala divai haikuingia kinywani mwangu, wala*

*sikujipaka mafuta kabisa,* ***hata majuma matatu kamili yalipotimia.****"*

**Mt 4:2 (SUV),** *"Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa."*

**Matendo ya Mitume 12:5**, *"Basi Petro akalindwa gerezani, nalo kanisa likamwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake."*

- Hata saa moja
- Usiku kucha
- Mara tatu kwa siku moja
- Siku tatu
- Siku ishirini na moja
- Siku arobaini

- Muda usiojulikana

Unaomba na kuwekeza muda kwenye hilo ombi? Jaribu kujifunza kwa watu wa michezo na Sanaa. Ili uwe mbobevu kwenye Nyanja husika, wamejifunza na hufanya hivyo – kuwekeza muda mwingi kufanya jambo hilohilo tena na tena bila kuchoka.

Kisa cha kanisa kuomba kwa ajili ya Petro alipokamatwa na kufungwa kinanionyesha ni kwa jinsi gani kanisa lilikuwa na juhudi katika kuomba sawa na Matendo ya Mitume 12:5. Hapa walichagua kuomba mpaka tu pale jibu

litakapopatikana… hakuna muda maalum!

Watu wanaochoka mapema katika maombi ni wavivu tu!

Ni kweli ulimaanisha hicho unachokiomba? Basi, dhihirisha kwa uwekezaji wa muda katika maombi na kumlilia Bwana.

## Kilio na Machozi

*“Yeye, siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti,* ***maombi na dua***

***pamoja na kulia sana na machozi,*** *akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu;"* Waebrania 5:7

Hapa anayezungumziwa ni Bwana Yesu Kristo mwenyewe. Mwanzilishi na mtimilizaji wa imani yetu. Kuna vitu alivitoa:

- Maombi
- Dua
- Kulia
- Machozi

Sasa, kwa kuwa mimi ni mwalimu wa neno la Mungu sitakuacha vivi hivi kwenye andiko hilo. Ninataka uone

mwandishi amegawanya hayo mambo kwenye makundi makubwa mawili: Mosi, ni kundi la maombi na dua kisha kuna neno linatumika hapo “pamoja na” ndipo tunapata kundi la pili, kulia sana na machozi!

Hapo utaona kuna nini; yaani, tendo na yaliyomo (maombi na dua) kisha utaona kuna namna ya uwasilishaji. Hapa ninaamisha ni kwa jinsi gani tendo na yaliyomo viliwasilishwa.

Kwa hiyo Bwana Yesu alitoa maombi na dua kwa njia ya kulia sana na machozi! Kulia sana na machozi si maombi bali ni njia ya kuwasilisha maombi… ndiyo

onyesho jenyewe sasa la bidii katika maombi.

Kama mchungaji, huwa ninamashaka sana na watu wanaomaliza muda mrefu (mathalani mwaka) wasiolia sana na kutoa machozi katika maombi. Haya ni maoni yangu binafsi na si msimamo wa moja kwa moja wa Biblia.

*"Basi Hezekia akajigeuza, akaelekeza uso wake ukutani, akamwomba BWANA, 3akasema, Ee BWANA, kumbuka haya, nakusihi, kwamba nimekwenda mbele zako katika kweli na kwa moyo mkamilifu, na kutenda yaliyo*

*mema machoni pako. Hezekia* ***akalia sana sana.*** *"* Isaya 38:2-3

Ingetosha kabisa kufahamu kwamba Hezekia alilia… na ingetosha tu kufahamu kwamba alilia sana. Lakini kwamba alilia san asana inainua umakinifu wa masikio yangu ya kujifunza.

Waza namna hii, ukienda msibani au mahali ambapo watu wanalia: Je, unaweza kusema tofauti katika ya makundi haya matatu ya watu:

- Wanaolia
- Wnaolia sana

- Wnaolia sana sana

Hiyo ikuelezee ni kwa namna gani Hezekia alilia!
Unahitaji ufunua gani zaidi ya kuchukua haya na kuyaweka kwenye utelekezaji?

**Kuhusu Mwandishi:**

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor, Priscilla na Butogwa; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: Pastor James Kalekwa

Instagram: @pastorjameskalekwa

Youtube: Pastor James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

## Ratiba za Ibada

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor ,Priscilla na Butogwa. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764

jameskalekwa.com